

CMA Anthem - Mlinzi Wake Maria

1 Mlinzi wake maria, mema mengi yako, Leo tumefahamu, mlinde mtoto wako.

***Kiitikio:* Mlinde mlinde mtoto wako x2**

2 Akija Rabi kwetu, ashukia kwako, Hana kaya kwa watu, ila nyumba yako.

3 Mle bandani kwa nyama, ulikuwa huko, uliyemlinda mama, mlinde mtoto wako.

4 Ukamlisha mwokozi, ndio kazi yako, Baba yake mkombozi, mlinde mtoto wako.

5 Watokapo askari, mtoto yesu hako, Ulimchukuwa misri, mlinde mtoto wako.

6 Ee yosefu myenyekevu, kwa msaada wako, Tupewe wokovu, mlinde mtoto wako